# HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE
(MKOA WA MARA)

JARIDA TOLEA LA KWANZA | AGOSTI-NOVEMBER 2023

KWANGWA, MUSOMA-MARA

www.musomarrh.go.tz



**DKT. OSIMUND DYEGURA**
**MGANGA MFAWIDHI**

**KARIBU KATIKA JARIDA TOLEO LA KWANZA KUANZIA MWEZI AGOSTI HADI NOVEMBA 2023, JARIDA LIMEANGAZIA MATUKIO MBALIMBALI YALIYOFANYIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE TOKEA MWEZI WA NANE (08) HADI MWEZI WA KUMI NA MOJA (11) 2023**



www.musomarrh.go.tz

# YALIYOMO

MUUGUZI MKUU WA SERIKALI HAIMIZA MAADILI KWA WAUGUZI NA WAKUNGA.

MADAKTARI BINGWA WA MACHO KUTOKA HOSPITALI YA KANDA BUGANDO-MWANZA WATOA HUDUMA YA UPIMAJI MACHO NA UPASUAJI KWA VIPINDI TOFAUTI TOFAUTI.

MKOA WA MARA WAPOKEA VIFAA TIBA NA MAGARI 31 IKIWEMO AMBULANCE 20 RC MTANDA AMSHUKURU RAISI SAMIA.

**HABARI PICHA**

SHIRIKA LA POSTA MKOA WA MARA LATOA ZAWADI WODI YA WATOTO NJITI

WAUGUZI NA WAKUNGA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA MJINI WAPATA MAFUNZO YA SHERIA NA MAADILI.

**HABARI PICHA**

MREJESHO WA MAFUNZO YA MFUMO MPYA WA UNUNUZI KATIKA TAASISI ZA UMMA (NEST)

ELIMU YA UGONJWA WA SICKLE CELL (SELIMUNDU) YATOLEWA MASHULENI

UHAKIKI WA UTAFITI ULIYOFANYWA NA CHUO CHA USTAWI WA JAMII DAR ES SALAAM

TMDA WATOA MAFUNZO ENDELEVU YA UCHUNGUZI WA AWALI WA MADAWA KATIKA MAABARA NDOGO HAMISHIKA

BODI YA USHAURI YA HOSPITALI YA WILAYA YA SERENGETI YAFANYA ZIARA YA MAFUNZO

MAFUNZO YA MFUMO WA AFYACARE

KIKAO CHA MABORESHO YA HUDUMA ZA AFYA (QIT)

MAHADHIMISHO YA SIKU YA UONI DUNIANI

KUMBUKUMBU YA KIFO CHA HAYATI BABA WA TAIFA MWALIMU J.K NYERERE.

# Muuguzi Mkuu wa Serikali ahimiza maadili kwa Wauguzi na Wakunga.

Muuguzi Mkuu wa serikali ambaye pia ni Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi na Ukunga nchini Tanzania ametoa wito kwa wakunga na wauguzi kufata taratibu na maadili ya uuguzi na ukunga ili kutoa huduma iliyo bora kwa wagonjwa.

Ameyasema hayo akiwa kwenye kikao pamoja na wauguzi na wakunga katika Hospitali ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwalimu J.K Nyerere siku ya 16/08/2023 alipokuwa akifanya ziara ili kukagua huduma za uuguzi na ukunga zinavyofanyika katika Hospitali ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwalimu J.K Nyerere.





"Muuguzi anatakiwa kuwa smart na kuangalia taratibu zilizopo na kufuata maadili ya uuguzi na ukunga ili kutoa huduma bora kwa wagonjwa"

Pia Muuguzi Mkuu wa serikali aliwasisitizia na kuwasihi wauuguzi na wakunga kuweza kujiendeleza kielimu ili kuongeza ubora pale wanapokuwa kwenye majukumu yao ya uuguzi na ukunga.

Katika kikao hicho pia aliwasisitizia wauguzi na wakunga swala la leseni na kusema katika sekta ya afya ni lazma kuwa na leseni ilithibitihswa na msajili wa Baraza la Ukunga na Uuguzi, Hivyo aliwaomba wale wote ambao leseni zao zimeisha muda wake waende wakauishe ili isije kuwa tatizo badae.

Moja ya swali lililoulizwa katika kikao hicho ni kuhusu posho ya sare ambazo wanavaa wauguzi na wakunga kuwa ni ndogo na swali hilo lilitolewa ufafanuzi na Muuguzi Mkuu wa serikali ambaye pia ni Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi na Ukunga nchini Tanzania, alisema kuwa swala hilo ya sare wanalifanyia kazi na likikamilika watalitolea majibu.



**Madaktari Bingwa wa Macho kutoka Hospitali ya kanda Bugando-Mwanza watoa huduma ya upimaji Macho na upasuaji kwa wakazi wa Mkoa wa Mara na maeneo jirani kwa vipindi tofauti tofauti.**

Madaktari bingwa wa macho kutoka Hospitali ya kanda ya Bugando-Mwanza katika vipindi tofauti tofauti wametoa huduma ya kibingwa ya matibabu ya macho pamoja na upasuaji kwa wananchi wa Mkoa wa Mara na maeneo jirani.

Huduma hiyo iliotolewa na Madaktari Bingwa kutoka Hospitali ya Knada ya Bugando-Mwanza wakishirikiana na Madaktari waliyopo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

Huduma hiyo ya macho ilitolewa kwa vipindi vitatu kuanzia mwezi wa nane mwaka 2023 kuanzia tarehe 14/08/2023 hadi tarehe 18/08/2023, mwezi wa tisa kuanzia tarehe 25/09/2023 hadi tarehe 29/09/2023 na mwezi wa kumi na moja kuanzia tarehe 20/11/2023 hadi tarehe 24/11/2023.

Huduma hizo za Macho kutoka kwa Madaktari Bingwa kutoka Hospitali ya kanda ya Bugando-Mwanza iliambatana na elimu ya utunzaji macho baada ya upasuaji.

Wananchi mbalimbali walijitokeza katika kambi hizo za madaktari Bingwa wa macho walipewa huduma ya vipimo pamoja na upasuaji kwa wale waliyokutwa na matatizo mbalimbali kwenye macho yao na pia waliishukuru Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kwa kuleta madaktari hawa na kusisitiza kuwa wanaomba wawe wanakuja kila mwezi..



**Mkoa wa Mara wapokea vifaa tiba na magari 31 ikiwemo ambulance 20 RC Mtanda amshukuru Raisi Samia.**

Mkuu wa Mkoa wa Mara Mhe. Said Mtanda leo Novemba 22 amezungumza na waandishi wa habari ofisini kwake na kuelezea namna Mkoa wa Mara ulivyonufaika na vifaa tiba vyenye thamani ya Tshs. 232,405,917.53 ambavyo vimepelekwa Kituo cha Afya Kisolya Wilayani Bunda pamoja na magari 31 yakiwemo magari ya kubebea wagonjwa (ambulance) 20 na magari ya usimamizi na ufuatiliaji 11.



Akizungumza na waandishi RC Mtanda amesema pamoja na vifaa tiba hivyo Mkoa wa Mara pia umepata vifaa tiba vyenye thamani ya Bilioni 4.8 kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya Mwal. J.K. Nyerere (Kwangwa).

Aidha Mhe. Mtanda amemshukuru Mhe. Rais Samia kwa upendo wake kwa wananchi wa Mkoa wa Mara kwa kukabidhi magari pamoja na vifaa tiba na-kuwataka Wataalamu wa sekta ya afya kuvitunza na kusimamia vyema vifaa tiba hivyo ili vitumike kama adhma ya Mhe. Rais Samia alivyodhamiria.



Mkuu wa Mkoa wa Mara Mhe. Said Mohamed Mtanda akiwa na Mganga Mfawidhi Dr. Osmund January Dyegura wakisalimiana na moja ya Mwanachi aliyekuja Hospitali kutibiwa.

# HABARI PICHA



**Huduma ya upimaji magonjwa yasiyokuwa yakuambukizwa imetolewa kwenye viwanja vya ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara siku ya tarehe 25/10/2023.**

Huduma ya upimaji wa Magonjwa yasiyokuwa ya kuambukizwa imetolewa siku ya jana katika viwanja vya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara.

Zoezi la upimaji Magonjwa yasiyokuwa ya kuambukizwa liliambatana na upimaji macho pamoja na upimaji wa virusi vya ukimwi kutoka kwa watoa huduma na Madaktari Hospitali ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwalimu J.K Nyerere. Huduma hiyo ilihusisha watumishi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Taasisi na Mashirika mbalimbali ya kiserikali pamoja na wananchi mbalimbali waliyokuwa eneo hilo.

Huduma zilizokuwa zikitolewa zilikuwa ni kama ifuatavyo:
1) Upimaji wa kisukari
2) Shinikizo la Damu
3) Urefu na uzito
4) Ushauri
5) Upimaji Macho
6) Upimaji wa virusi vya ukimwi

## Shirika la Posta Mkoa wa Mara latoa zawadi wodi la watoto njiti



Kila tarehe 09 oktoba ya kila mwaka shirika la Posta huadhimisha siku ya Posta Duniani, katika kuadhimisha siku ya Posta Duniani Shirika la Posta Mkoa wa Mara lilitoa zawadi kwa wazazi waliyojifungua watoto njiti Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

Zawadi zilizotolewa ni sabuni na pampers kwa wamama ishirini na tano (25).

## Wauguzi na wakunga Halmashauri ya Manispaa ya Musoma Mjini wapata mafunzo ya sheria na maadili.

Wauguzi na Wakunga wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma Mjini walipata Mafunzo ya Sheria na maadili katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, siku ya jumanne ya tarehe 10/10/2023 ili kuwakumbusha wauguzi na wakunga kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria na maadili ya Uuguzi na Ukunga.

Mafunzo hayo yaliendeshwa na Mwanasheria kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bw. Isaya Nkya, Pamoja na Bi. Mwajuma Mutabazi Afisa Muuguzi Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania.

Hayo yalijiri baada ya Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Agnes Mtawa kufanya ziara katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma Mjini ili kuona utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Uuguzi na Ukunga zinavyotekelezwa.





# HABARI PICHA








Habari picha wananchi mbalimbali mkoa wa Mara na maeneo jirani walijitokeza kwa ajili ya matibabu kutoka kwa Madaktari Bingwa Hospitali ya Kanda Bugando.

Kambi ya Madaktari Bingwa kutoka Hospitali ya Kanda ya Bugando-Mwanza kwa kushirikiana na Madaktari waliyopo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ilifanyika kwa vipindi viwili kuanzia tarehe 04/09/2023 hadi 08/09/2023 pamoja na tarehe 02/10/2023 hadi tarehe 06/10/2023.

Kambi hii inahusisha Madaktari Bingwa wa;

1.Daktari Bingwa wa ngozi (Dermatologist).
2.Daktari Bingwa wa Magojnwa ya Ndani (Physician).
3.Daktari Bingwa wa sikio, pua na koo (ENT Surgeon).

## Mrejesho wa Mafunzo ya mfumo mpya wa ununuzi katika taasisi za umma (NeST)

Siku ya tarehe 08/09/2023 ulitolewa mrejesho wa mafunzo ya mfumo mpya wa ununuzi katika taasisi za umma (NeST). Mawasilisho hayo yaliwasilishwa na Afisa Ugavi Msaidizi Event Mwenzegule.



Mafunzo ya mfumo mpya wa ununuzi katika taasisi za umma yalifanyika Mkoani Iringa kwa siku tano kuanzia tarehe 28/08/2023 hadi 01/09/2023, Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ilitoa wawakilishi watatu kuhudhuria mafunzo hayo ambao ni kutoka Ofisi ya ugavi, Ofisi ya uhasibu Pamoja na ofisi ya Tehama.
Mfumo wa NeST umeanzishwa mahususi kwa ajili ya ununuzi katika taasisi zote za serikali.

## Elimu ya ugonjwa wa sickle cell (selimundu) yatolewa mashuleni





Katika kuadhimisha siku ya Seli Mundu duniani Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere iliadhimisha kwa kutembelea shule mbalimbali za sekondari silizopo Wilaya ya Musoma na kutoa elimu juu ya ugonjwa wa Seli Mundu kwa wanafunzi.



Maadhimisho hayo yaliambatana na mazoezi mbalimbali kama vile upimaji presha, utoaji elimu lishe, upimaji sukari na uchangiaji damu salama.

Shule zilizotembelewa ni kama vile shule ya sekondari ya wasichana, shule ya ufundi musoma sekondari ya wavulana na kigera sekondari.

Maadhimisho ya Seli Mundu duniani hufanyika mwezi wa tisa ya kila mwaka.

## Uhakiki wa utafiti uliyofanywa na chuo cha ustawi wa jamii Dar es salaam



Siku ya tarehe 24/10/2023 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kulifanyika uhakiki wa ripoti ya utafiti uliyofanywa na chuo cha ustawi wa jamii kilichopo Dar es salaam kuhusu Mila na Desturi zinazomlinda Mwanamke dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Ripoti hiyo iliwasilishwa na Dkt. William Manyama Mhadhiri Mwandamizi kutoka cguo cha ustawi wa jamii Dar es salaam. Utafiti huo umefanywa kuanzia mwaka 2022 huku ukihusisha mikoa ya Mara, Tanga na Mbeya.

Kwa mujibu wa Dkt. William Manyama Mhadhiri Mwandamizi amesema kuwa utafiti huo umelenga wazee kwasababu ya uzoefu na ndiyo kundi linalojua zaidi mila na desturi.



## TMDA watoa mafunzo endelevu ya uchunguzi wa awali wa madawa katika maabara ndogo hamishika




Tarehe 31/10/2023 TMDA watoa mafunzo endelevu ya uchunguzi wa awali wa madawa katika maabara ndogo hamishika Hospitali ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwalimu J.K Nyerere kwa wafamasia.



Mafunzo hayo yameendeshwa na Babuali Ahmed pamoja na Abdallah Juma ambao ni wataalam wa maabara kutoka TMDA Minlab Makao Makuu Dar es salaam.

Babuali Ahmed Mtaalam wa Maabara kutoka TMDA Minlab amesema kuwa "Lengo la ziara ilikuwa ni kutoa mafunzo mafupi na kuangalia changamoto katika kituo hiki kwasababu kituo hiki ni moja kati vituo 23 vya Maabara hamishika vinavyosimamiwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba ikiwa na lengo la kusimamia dawa na kuhakikisha kwamba watumiaji wanatumia dawa zenye ubora stahiki

## Bodi ya ushauri ya Hospitali ya Wilaya ya Serengeti yafanya ziara ya mafunzo




Siku ya tarehe 24/10/2023 Bodi ya ushauri ya Hospitali ya Wilaya ya Serengeti ilifanya ziara ya mafunzo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

Ziara hiyo ya mafunzo ililenga kujifunza mbinu mbalimbali za uendeshaji wa Hospitali katika maeneo tofauti tofauti kama vile kazi za utawala, ustawi wa jamii Pamoja na kazi za baadhi ya Idara za hospitali ili kuweza kuongeza ufanisi katika hospitali yao.

Aidha Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Serengeti Dr. Mohere Mohere alisema kuwa lengo lao kubwa kufanya ziara hiyo ya mafunzo ni kujifunza haswa maswala ya kiutawala, mifumo ya ukusanyaji mapato na matumizi na huduma za utoaji misamaha haswa makundi maalum.






## Mafunzo ya mfumo wa afyaCare







Picha hapo juu zinaonyesha matukio mbalimbali ya mafunzo ya mfumo wa AfyaCare unaotumika kuingizia taarifa za wagonjwa, Mafunzo ya mfumo wa Afya Care yalichukua siku takribani tisa kuanzia tarehe 04/09/2023 hadi siku ya tarehe 13/09/2023.



Mafunzo ya mfumo wa afyacare yaliendeshwa chini ya Maafisa Tehama kutoka wizara ya afya.

## Kikao cha maboresho ya huduma za afya







Katika kuendelea kuimarisha utoaji huduma bora za matibabu kwa wananchi, timu ya maboresho (QIT) ilifanya kikao kwa lengo la kuibua changamoto mbalimbali zinazojitokeza wakati wa utoaji huduma za afya kwa wananchi na namna kutatua changamoto hizo maeneo mbalimbali ya taasisi.

Kikao hiki kilikaliwa siku ya tarehe 16/11/2023.

## Mahadhimisho ya siku ya uono duniani








Katika kuadhimisha siku ya uono Duniani iliyofanyika siku ya tarehe 12/10/2023, watoa Huduma wetu walifika CRDB & NMB tawi la Musoma Mjini na kutoa elimu juu ya utunzaji Macho kwa wafanyakazi.

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kwa ujumla iliadhimisha siku hii kwa kutoa huduma za kupima macho, kutoa elimu ya afya ya macho na namna ya kuepuka visababishi vinavyosababisha kupunguza uono wa macho.

## KUMBUKUMBU YA KIFO CHA HAYATI BABA WA TAIFA MWALIMU J.K NYERERE.

Kila tarehe 14/10/2023 huwa ni kumbukumbu ya kumuenzi Hayati Baba wa Taifa Mwalimu J.K Nyerere, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere imeendesha zoezi la upimaji magonjwa yasiyo ya kuambukiza na uchangiaji wa Damu Salama katika viwanja vya SDA Mukendo.

Zoezi hili la upimaji magonjwa yasiyo ya kuambukiza na uchangiaji wa Damu salama lilikamilika tarehe 15/10/2023 katika viwanja vya KKKT-Nyasho.







# AFYA YAKO NDIYO DHAMIRA YETU

TUNAPATIKANA KWANGWA HALMASHAURI YA MANISPAA
YA MUSOMA MJINI MKOA WA MARA




TUFATILIE KWENYE KURASA ZETU

hospitali ya mwalimu nyerere

hospitali_ya_mwalimu _nyerere

www.musomarrh.go.tz

nyerereafyatv